**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**
**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


Namba za simu

Shule ya Sekondari Lugufu Girls,

S .L. P 12,

KIGOMA- UVINZA

Mkuu wa shule: 0767 505902

Makamu mkuu wa shule: 0625 616936

Mtaaluma wa shule: 0620 812906

Mwalimu wa nidhamu: 0621 444160

Website: lugufugirlsschool.ac.tz


**Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi; ………………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUGUFU GIRLS HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA MKOA KIGOMA MWAKA 2024**

1. Ninafurahi Kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii, atasoma tahasusi ya ………………….
   Shule ya sekondari Lugufu Girls ipo umbali wa kilomita 12 kusini mwa makao makuu ya wilaya ya uvinza panapoitwa Lugufu.
   Kwa wanaosafiri na gari (bus) kutokea mikoa ya Dar-es-salaam, Morogoro, Dodoma, mikoa ya kaskazini na kwingineko kwenda Kigoma kupitia Tabora, watashuka sehemu inayoitwa LUGUFU POLICE (wilaya ya Uvinza), hapo watapanda pikipiki (bodaboda) hadi shuleni kwa gharama ya Tsh. 5,000/=. Ukishukia kituo cha Uvinza gharama za usafiri wa bodaboda itaongezeka. Kwa watakaosafiri na usafiri wa treni/garimoshi (Train) watashuka Uvinza, hapo watapanda daladala ziendazo Kigoma mjini na watashuka LUGUFU POLICE, nauli ni Tsh. 2,000/= toka Uvinza hadi Lugufu police kwa daladala.
   Na kwa watakaotokea Kigoma mjini, watapanda gari za kwenda Uvinza na watashuka LUGUFU POLICE, nauli ni Tsh. 4,000/= toka Kigoma mjini hadi Lugufu police kwa daladala.

2. **Mambo ya kuzingatia**

**2.1 SARE ZA SHULE**

i. Sketi nyeusi mbili zenye Linda box kubwa mbele moja na nyuma moja, linda ndogo ndogo kulia 2 na kushoto 2, sketi ziwe ndefu hadi kufika chini kabisa (ziguse ankle) na tai nyeusi ndefu.
ii. Sketi mbili za kushindia rangi ya zambarau zenye malinda na ndefu kama sketi nyeusi na t-shirt mbili au zaidi za bluu round collar (kola). T-shirt hizi anaweza kuzipata shuleni kwa gharama nafuu.
iii. Mashati mawili meupe mikono mirefu yenye kola.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya visigino vifupi na vyenye kamba na soksi nyeupe.
v. Sweater la kijani ya kijeshi (dark green), anaweza kulipata shuleni kwa gharama ya Tsh. 15,000/= au anunue aje nalo.
vi. T-shirt ya shule rangi ya kijani yenye kola na nembo ya shule, anaweza kuipata shuleni kwa gharama ya Tsh. 13,000/= au anunue aje nayo.
vii. Track suti nyeusi yenye michirizi/mistari myeupe pembeni kwa ajili ya baridi na kujisomea usiku.
viii. Viatu aina ya raba na jezi (jersey) nyeusi yaani t-shirt na bukta isiyobana yenye mistari myeupe pembeni kwa ajili ya michezo.
ix. Gum boot kwa ajili ya matope vipindi vya mvua

**N.B Kwa wanafunzi wanaovaa ijabu, aje na ijabu nyeupe kwa ajili ya darasani na Ijabu nyeusi kwa kushindia ambazo ni ndefu za kufunika mikono. Zisiwe na mapambo ya aina yoyote.**

**kwa sare (uniform) zote atakazokuja nazo ziwe zimeandikwa (printed) majina yake mwanafunzi. Mwanafunzi yeyote asije na nguo za nyumbani.**

**2.2 MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO**

a. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Karatasi ya matokeo ya mwanafunzi ya kidato cha nne (form four result slip) original na copy, na nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.
ii. Ream za karatasi mbili (2) kwa kila mwaka – A4. Kwa muhula ni ream moja (1)
iii. Shuka mbili (2), rangi ya pink na branket moja (1) na chandarua rangi ya bluu
iv. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,kijiko na kikombe)
v. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko, dumu la lita tano (5) kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa pamoja na beseni la kufulia.
vi. **PCB** na **HGK** aje na mop (kifaa cha kudekia floo) pamoja na squeegee (squeezer), **CBG, HKL & HGL** aje na jembe lenye mpini pamoja na hard broom (brush), **HGE, HGLi & HGFa** aje na jembe lenye mpini, panga pamoja na ufagio wa chelewa.
vii. Godoro moja (1) futi 3 kwa 6. Pia yanapatikana shuleni kwa gharama nafuu.
viii. Kamusi ya Kiswahili sanifu moja (1) kwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili na kamusi ya kiingereza (English advanced learners dictionary) kwa wanafunzi wanaosoma English language na wengine pia.
ix. Aje na vitabu vinavyohusisha masomo yake.
x. Scientific calculator kwa michepuo ya **HGE, PCB & CBG**, na Graph pad 1 kwa **CBG, PCB,HGL,HGK, HGE, HGLi na HGFa.**
xi. Dissecting kit kwa **PCB** na **CBG**.
xii. Box file ndogo kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka zake mbalimbali za darasani.

xiii. Tochi ya solar kwa ajili ya matumzi yake ya kujisomea kipindi ambacho umeme unakata.
xiv. Sanduku la chuma (trunk) kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.
xv. Taulo/kitenge/khanga
xvi. Tsh. 6,000/= kwa ajili ya kukatiwa bima ya afya. (aje nayo mkononi, isiingizwe bank)
xvii. Sabuni ya kufulia na kuogea pamoja na mahitaji mengine madogomadogo ikiwemo pesa ya matumizi ya mtoto (pocket money)

## 3. MICHANGO MBALIMBALI

### a) Shule za bweni

| **Na.** | **Aina ya mchango** | **kiasi** |
|---|---|---|
| **1** | Mchango wa uendeshaji shule | 65,000/= |
| **2** | Tahadhali | 5,000/= |
| **3** | Nembo | 5,000/= |
| **4** | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii iingizwe kwenye akaunti ya shule(hatupokei mkononi)**
**Namba ya akaunti…………. 51601100089**
**Jina la akaunti …………….. Lugufu Girls Secondary School**
**Benki ………………………. NMB**
Mwanafunzi aje na slip ya malipo ya benki kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za shule.

## 4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

**4.0.** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**4.1. Sheria na kanuni za shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Pia, kipindi chote mwanafunzi awapo shuleni hataruhusiwa kuongea na mzazi/mlezi wake moja kwa moja kupitia simu yoyote ile bali mawasiliano baina ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yatafanyika kupitia mwalimu wa mawasiliano wa mwanafunzi husika. Namba za mwalimu wa mawasiliano zitatolewa na mkuu wa shule pindi mwanafunzi atakaporipoti.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule (msiba au ugonjwa)**
-

**4.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule**

1) Wizi.
2) Kutohudhuria masomo kwa muda wa siku 90 bila taarifa (utoro).
3) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.
5) Kupigana mwanafunzi na mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
6) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
7) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
8) Uvutaji sigara.
9) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuolewa.
10) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
11) Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
13) Kumiliki, kukutwa na kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
14) Kudharau bendera ya taifa.
15) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
16) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**5. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni, ulipaji michango na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni (kila jumamosi ya mwisho wa mwezi) pamoja na namba zao za simu.
e) Orodha ya vitabu vilivyopendekezwa na shule.

NB: tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## MAELEZO MUHIMU

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama ni walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wao anaumwa yuko mahututi hivyo mzazi/mlezi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KWA KUPIGIWA SIMU AU UJUMBE MFUPI WA MANENO KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**

- **Mkuu wa shule 0767 505 902**
- **Makamu mkuu wa shule 0625 616 936**
- **Mtaaluma mwandamizi 0620 812 902**
- **Mlezi mwandamizi 0621 444 160**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**…………………………..**
**JEMIMA Y. YUSTO**
**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI LUGUFU GIRLS**
**S. L. P 12, UVINZA**
**FORM NUMBER 1.**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To medical officer I/C of …………………………………………………………………………

Designated Hospital, P. O. Box ………………………………………………………..

Please examine the above named in full as to her physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. The examination should include categories a-m.

In case of any acute or defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to school of students with special needs.

a) Student’s name ………………………………………………..
b) Age …………………………………..
c) Stool test …………………………………………………………………………..
d) Blood group ………………………………………………
e) Urine analysis …………………………………………………………………..
f) Syphilis test ……………………………………………………………………………….
g) Chest test …………………………………………………………………………..
h) Speech ……………………………………………………………………………..
i) Eye test …………………………………………………………………………………….
j) Abdomen ……………………………………………………………………………
k) Chest X-ray ………………………………………………………………………….
l) Sickle cell test …………………………………………………………………….
m) WCB total Differential ………………………………………………………………...
Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………..

Signed by ……………………………………………………………

Designation ………………………………………………………..

Official stamp

Date :

**SHULE YA SEKONDARI LUGUFU WASICHANA**
**S. L. P 12, UVINZA**
**FORM NUMBER 2.**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

i. Jina la mwanafunzi ………………………………………………………………..
ii. Jina la baba ……………………………………………………………
iii. Jina la mama ………………………………………………………..
iv. Jina kamili la mlezi ………………………………………………….
v. Anuani ya mzazi/mlezi …………………………………………..
vi. Uhusiano wa mlezi ……………………………………………….
vii. Kazi ya baba. (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi n.k). ……………………………
viii. Kama ni mkulima, zao muhimu analolitegemea ni …………………………………….
ix. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni ……………………………………….
x. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni ……………………………………………….
xi. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi……………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
… ………………………………………………………………………………
xii. Madhehebu ya dini …………………………………………………..
xiii. Jamaa ya ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi

| jina kamili | kazi yake | namba ya simu | |
|---|---|---|---|
| 1 ………………………………… | ……….………………….. | …………………………. | Bandika picha |
| 2 …………………………………. | ………………………... | ………………………… | Bandika picha |
| 3 ………………………………... | …………………………… | …………………………. | Bandika picha |
| 4 ………………………………. | ……………………………. | …………………………. | Bandika picha |

**SHULE YA SEKONDARI LUGUFU WASICHANA**
**S. L. P 12, UVINZA**
**FORM NUMBER 3**
**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Jina la mwanafunzi ……………………………………………………..

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………………..

Anuani ya mzazi/mlezi …………………………………………………

Uhusiano ………………………… (Mfano; baba, mjomba, kaka, dada n.k)

Mimi …………………………………………………… nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zangu zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………….. tarehe ……………………

Mimi ………………………………. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi …………………………………
ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.
Sahihi ya mzazi/mlezi ………………………………….. tarehe …………………………..

**ORODHA YA VITABU VILIVYOPENDEKEZWA NA SHULE**

1. ECONOMICS.
    i. Economics I Alive paper 1 & 2 by Zist Kamili
    ii. Economics for Advanced Level Paper 1 & 2 by C.M Ambilikile
    iii. Essentials for A- level Economics paper 1 & 2 by Ambrose Odhiambo
2. GEOGRAPHY
    i. Physical geography for secondary school. Revised edition (2019) by Msabila D.T
    ii. Physical geography for secondary schools and colleges by Zisti Kamili
    iii. Practical geography for secondary school.(2016) by Zist Kamili.
    iv. Human and Economics geography by D.T Msabila (geography 2)
3. HISTORY
    i. Contemporary Historical Events (2013) by Tumain C. Shibital. history 1 & 2
    ii. Essential In Advanced Level History 2015 (2015) by Saleh Yasin. History 1 & 2
    iii. Zist kamili History 1 & 2
4. KISWAHILI
    i. Nadharia ya lugha by Masebo & Nyambari Nyangwine
    ii. Nadharia ya fasihi by Masebo & Nyambari Nyangwine
    iii. Nadharia ya lugha by C. Saluhaya
    iv. Nadharia ya fasihi by C. Saluhaya
    v. Tahakiki ya vitabu teule (kidato cha 5 & 6) by Nyambari Nyangwine
5. ENGLISH LANGUAGE
    i. Advanced level English Language by Shadrack Ndambo & James Kinunda (English language 1)
    ii. Advanced level English Language by Nicholous Ashel ( English language 1)
    iii. Advanced level literature by Nicholous Ashel (English language 2)
    iv. The analytical analysis of Advanced literature by Mgonja, M.E (English language 2)
    v. Advanced level literature by Nyambari Nyangwine (English language 2)
6. BIOLOGY
    i. Biological science 1 & 2 (third edition)
    ii. Understanding biology
    iii. Biology for Advanced level secondary schools by TIE.

7. CHEMISTRY
    i. Conceptual chemistry by S. Chand. (chemistry 1 & 2)
    ii. Chemistry for Advanced level secondary school -Physical chemistry -General chemistry -Organic chemistry -Inorganic chemistry
    iii. Hopegen series book by Ngaiza -Physical chemistry -General chemistry -Organic chemistry -Inorganic chemistry -Soil chemistry for Advanced level
8. PHYSICS
    i. Principles of Physics, by Chand S (7th Edition)
    ii. Advanced level Physics by Roger Mun Caster (4th Edition)
    iii. Nelkon and Palker